

Mkate wa Siku

NENO LA SIKU

APRILI 2022

SIKU

30

SIKU 01 – HAGAI 1:13b (SUV)

"Mimi nipo pamoja nanyi, asema BWANA."

SIKU 02 – ZAKARIA 10:1a (BHN)

"Mwombeni Mwenyezi-Mungu awape mvua za masika. Mwenyezi-Mungu ndiye aletaye mawingu ya mvua ..."

SIKU 03 – ZABURI 16:11 (SUV)

"Utanjulisha njia ya uzima; Mbele za uso wako ziko furaha tele; Na katika mkono wako wa kuume Mna mema ya milele."

SIKU 04 – YOHANA 1:16 (BHN)

"Utanjulisha njia ya uzima; Mbele za uso wako ziko furaha tele; Na katika mkono wako wa kuume Mna mema ya milele."

SIKU 05 – ISAYA 40:1 (RSV)

"Watulizeni mioyo, watulizeni mioyo, watu wangu, asema Mungu wenu."

SIKU 06 – 2 WAKORINTHO 12:9 (NEN)

"...Neema yangu inakutosha, kwa kuwa uweza wangu hukamilika katika udhaifu."...

SIKU 07 – 2 SAMWELI 7:29b (SUV)

"... kwa maana wewe, Ee Bwana MUNGU, umelinena na kwa baraka yako nyumba ya mtumwa wako na ibarikiwe milele."

SIKU 08 – ZABURI 44:8 (BHN)

"Daima tutaona fahari juu yako, ee Mungu; tutakutolea shukrani milele."

SIKU 09 – ISAYA 45:2a (ONEN)

"Nitakwenda mbele yako na kusawazisha milima; nitavunjavunja malango ya shaba na kukatakata mapingo ya chuma."

SIKU 10 – DANIELI 2:21 (NEN)

"Yeye hubadili nyakati na majira; huwaweka wafalme na kuwaondoa. Huwapa hekima wenye hekima, na maarifa wenye ufahamu."

SIKU 11 – 2THESSALONIKE 3:16a (RSUV)

"Sasa, Bwana wa amani mwenyewe na awape amani daima kwa njia zote..."

SIKU 12 – KUMBUKUMBU 31:6b (SUV)

"... kwa maana BWANA, Mungu wako, yeye ndiye anayekwenda pamoja nawe, hatakupungukia wala kukuacha."

SIKU 13 – ISAYA 57:14b (BHN)

"Jengeni! Jengeni! Tayarisheni njia! Ondoeni vikwazo vyote njiani mwa watu wangu!"

SIKU 14 – WAEBRANIA 4:15 (NEN)

"Kwa kuwa hatuna Kuhani Mkuu asiyeweza kuchukuliana na sisi katika udhaifu wetu, lakini tunaye mmoja ambaye alijaribiwa kwa kila namna, kama vile sisi tujaribiwavyo: lakini yeye hakutenda dhambi."

SIKU 15 – 1 PETRO 2:24a (ONEN)

"Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, ili tufe kwa mambo ya dhambi, bali tupate kuishi katika haki..."

SIKU 16 – 1 YOHANA 4:9 (SUV)

"Katika hili pendo la Mungu lilionekana kwetu, kwamba Mungu amemtuma Mwanawe pekee ulimwenguni, ili tupate uzima kwa yeye."

SIKU 17 – WARUMI 5:1 (BHN)

"Sasa, kwa vile tumefanywa kuwa waadilifu kwa imani, basi tunayo amani naye Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo."

SIKU 18 – WAEFESO 2:4 (RSUV)

"Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda."

SIKU 19 – YOSHUA 1:18b (NEN)

"... Uwe imara na hodari tu!"

SIKU 20 – ZABURI 84:11a (BHN)

"Mwenyezi-Mungu ni jua letu na ngao yetu; yeye hutunemesha na kutujalia fahari."

SIKU 21 – WILUPI 4:13 (ONEN)

"Naweza kuyafanya mambo yote katika yeye anitiaye nguvu."

SIKU 22 – 1WAKORINTHO 16:13 (RSUV)

"Kesheni, simameni imara katika imani, iweni na ujasiri, mkawe hodari."

SIKU 23 – ISAYA 60:1 (NEN)

"Ondoka, angaza, kwa kuwa nuru yako imekuja na utukufu wa Bwana umezuka juu yako."

SIKU 24 – ZABURI 119:154 (BHN)

"Nitete katika hali hii yangu na unikomoe, uyahifadhi maisha yangu sawasawa na ahadi yako."

SIKU 25 – MAOMBOLEZO 3:56a (SUV)

"Ukaisikia sauti yangu; 'usifiche sikio lako'"

SIKU 26 – YEREMIA 31:25 (ONEN)

"Nitawaburudisha waliochoka na kuwatuliza walio na huzuni."

SIKU 27 – MITHALI 21:31 (NEN)

"Farasi huandaliwa kwa ajili ya siku ya vita, bali ushindi huwa kwa Bwana. "

SIKU 28 – KUTOKA 20:24b (BHN)

"Msiogope, maana Mungu amekuja kuwajaribu ili mpate kumcha yeye daima na msitende dhambi."

SIKU 29 – 1 PETRO 5:7 (SUV)

"huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu."

SIKU 30 – ZABURI 116:17 (BHN)

"huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu."

**Makala hii imechukuliwa
kutoka**

**www.biblesociety.ca © Haki
zote zimeifadhiwa.**

*Tunawashukuru sana kwa kuungana
na sisi kueneza Neno la Mungu hapa
Tanzania na duniani kote kwa ujumla.*

Chama cha Biblia cha Tanzania

16 Hatibu / 9 Barabara, Eneo la Madukani,
S.L.P 175, Dodoma - Tanzania

<https://shop.biblesociety-tanzania.org/>

<https://tanzanian.bible/>

<https://biblesociety-tanzania.org>



&



**Canadian
Bible Society**

10 CARNFORTH ROAD, TORONTO, ON M4A 2S4
TOLL FREE: 1.800.465.2425 EMAIL: INFO@BIBLESOCIETY.CA
WWW.BIBLESOCIETY.CA